

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA MOJA

22 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA MOJA – TAREHE 22 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**87. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA
THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaiongezea TARURA fedha ili iweze kuzihudumia barabara za Wilaya ya Kyerwa.

88. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itarudisha hekta elfu nane zilizopo kwenye Pori la Rwande Jimbo la Geita kwani pori hilo limepoteza sifa ya kuwa Hifadhi.

WIZARA YA KILIMO:

89. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kutatua changamoto zinazokabili miradi ya umwagiliaji ya Mkoga na Kitwiru iliyopo Manispaa ya Iringa.

90. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina Mkakati gani wa kupunguza bei za Mbolea zinazopanda kwa kasi kwenye Soko la Dunia ili kumpunguzia Mkulima mzigo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

91. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- Je, ni lini Serikali itajenga majosho ya mifugo katika Kata za Makilawa, Igelansoni, Iyumbu, Ighombwe, Mgungira na Mwaru Wilayani Ikungi.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

92. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara inayounganisha Wilaya ya Kyela na Ludewa kupitia Matema, Ikombe hadi Liuli itaanza kujengwa.

**93. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA
(KOROGWE VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli hadi Soni ambayo ilitengewa fedha utaanza.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**94. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE
SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu na TBC Redio katika Jimbo la Muhambwe.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

**95. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyanzo vya mitaji kwa Akinamama Wajasiriamali mbali ya fedha zinazotolewa na Halmashauri.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

96. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani kuirejeshea Halmashauri ya Liwale fedha za miradi zilizorudishwa Hazina ili kujenga Stendi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
22 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**